

UTUKUFU NI USUMBUFU

1. Sijauona pahali, hata na yake harufu
Sijasikia kauli, ilotoa majisifu
Utukufu kwamba kweli, usiwe na usumbufu
Sijaona utukufu, ukakosa usumbufu
2. Iwe kakupa Jalali, Unabii unyoofu
Au wa kiserikali, uongozi wa kichifu
Mashaka na uzohali, ni lazima yakukifu
Sijaona utukufu, ukakosa usumbufu
3. Walo na vyeo fadhili, na heshima ya turufu
Wenye nzito ratili, hadhi na uaminifu
Mikosi na uthakili, yawakumba yenye ghofu
Sijaona utukufu, ukakosa usumbufu
4. Mtume wetu Rasuli, kipenzi chake Raufu
Katika zake shughuli, za kuleta maongofu
Kakumbwa na idhilali, mikosi safu kwa safu
Sijaona utukufu, ukakosa usumbufu
5. Dhamana yastahili, utatue udhaifu
Uondoe mushkeli, huduma ziwe nadhifu
Ndipo adha na madhili, huja kama masurufu
Sijaona utukufu, ukakosa usumbufu
6. Unapovishwa medali, dhamana ya usanifu
Hangaiko wakabili, shida, mikosi na rafu
Usumbufu, ukatili, ndo jaza ya utukufu
Sijaona utukufu, ukakosa usumbufu

Bakari A. Ali
Zanzibar 1995